

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb.Na.MZA/KDC/S.10/40/80

26 Mei, 2023

**Yah: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za **Msaidizi wa Kumbukumbu II**. Tangazo hili linarekebisha Tangazo la nafasi za kazi lenye Kumb Na. MZA/KDC/S.10/40/78 la tarehe 20/04/2023 na Tangazo la kazi lenye Kumb.Na. MZA/KDC/S.10/40/79 la tarehe 27/04/2023 kutokana na Marekebisho ya Kisahihisho "C" cha Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.9 wa mwaka 2002 Kumb.Na.AB.260/472/01 ya tarehe 01/03/2023 kuhusu muundo wa Kada ya Wasaidizi wa Kumbukumbu.

Hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi zifuatazo:

**1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI MBILI (2)**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji anatakiwa awe mwenye Elimu ya Kidato cha Nne au Kidato cha Sita na Mwenye Stashahada (Diploma) ya Utunzaji Kumbukumbu (**NTA LEVEL 6**) katika mojawapo ya fani za Masjala au Afya.

**1.2 MAJUKUMU**

- i) Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajiwa na Watendaji/Action Officers.
- ii) Kudhibiti upokeaji na uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka
- iii) Kuorodhesha barua zinazolingia masjala kwenye rejista (incoming correspondence register)
- iv) Kuchambua , kuorodhesha na kupanga nyaraka katika majalada kulingana na somo husika (classification and indexing).
- v) Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi kwenye rejista (outgoing correspondence register).
- vi) Kusambaza majalada kwa Watendaji/Action Officers
- vii) Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi
- viii) Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filing cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa.
- ix) Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa Watendaji/Action Officers

**1.3 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali yaani TGS C.1

**1.4 MASHARTI YA JUMLA**

- i) Waombaji wawe ni Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- ii) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- iii) Waombaji wawasilishe picha ndogo mbili za hivi karibuni (passport size).
- iv) Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha "Result Slip", "Statement of Results", "Provisional Results" au "Transcripts" **HAVITAKUBALIKA.**
- v) Kwa Waombaji waliosoma nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha Nne au Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- vi) Kwa waombaji waliosoma Vyuo nje ya Nchi wawasilishe uthibitisho kutoka (NACTE).
- vii) Waombaji watakokidhi sifa zinazotakiwa ndio watakaoitwa katika usaili.
- viii) Waombaji waandike namba ya Kitambulisho cha Taifa katika barua zao za maombi ya kazi au waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- ix) Barua ya maombi iliyosainiwa na Mwombaji inawezakuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
- x) Waombaji wenye mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi yao.
- xi) Waombaji watakaowasilisha Taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.
- xii) Maombi yatakayoletwa moja kwa moja bila kupitia Posta hayatapokelewa.
- xiii) **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 06 Juni, 2023 saa 9:30 Alasiri. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anuani ifuatayo:**

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya.  
S.L.P. 88,  
NGUDU-KWIMBA.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovoti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba [www.kwimbadc.go.tz](http://www.kwimbadc.go.tz)

Tangazo hili limetolewa na;



Denis D. Kabogo

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

*MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA*